# *Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo*

## 1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 MEI, 2025 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 21-31 MEI, 2025

### 1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA TAREHE 11-20 MEI, 2025

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kudhoofika. Hali hii ilisababisha sehemu ya ukanda mvua kuendelea kuwepo katika nchi yetu, hususan katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Kwa upande mwingine Joto la bahari katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki) lilikuwa la juu kidogo ya wastani. Hali hii ilisababisha kuendelea kudumisha uwepo wa migandamizo midogo ya hewa na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani.

### 1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 MEI, 2025

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea kuwepo kwa vipindi vya mvua kubwa zilizoambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo ya nchi hususan yale yaliopo ukanda wa Pwani ya kaskazini, ukanda wa Ziwa Victoria na nyanda za juu kaskazini mashariki.

## 2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 21-31 MEI, 2025

### 2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 21-31 MEI, 2025

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhoofika. Hali hii inatarajiwa kusababisha sehemu ya ukanda mvua kuendelea kuwepo katika nchi yetu, hususan katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria. Kwa upande mwingine Joto la bahari katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki) linatarajiwa kuendelea kuwa la juu kidogo ya wastani. Hali hii inatarajiwa kuendelea kudumisha uwepo wa mgandamizo mdogo wa hewa na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 MEI, 2025**

**Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):** Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache hususan ya mkoa wa Kigoma.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Imetolewa na;

***MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA***

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz